LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# UKATILI WA KIJINSIA

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# UKATILI WA KIJINSIA

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO


**SHUKRANI ........................................ 5**

**1. Ukatili wa Kijinsia ........................................ 11**

1.1.Jinsi ni nini? ........................................ 11

1.2.Jinsia ni nini? ........................................ 11

1.3.Maana ya Ukatili ........................................ 11

1.4.Ukatili wa Kijinsia ........................................ 11

**2. Aina za ukatili wa kijinsia ........................................ 12**

2.1.Ukatili wa Kimwili ........................................ 12

2.2.Ukatili wa Kisaikolojia ........................................ 12

2.3.Ukatili wa Kiuchumi ........................................ 12

2.4.Ukatili wa Kiafya ........................................ 13

2.5.Ukatili wa Kingono ........................................ 13

**3. Sababu (Chanzo) zinazochangia Ukatili wa Kijinsia ........................................ 14**

**4. Athari za Ukatili wa Kijinsia ........................................ 14**

**5. Mwongozo wa utoaji huduma kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia ........................................ 16**

5.1.Hatua ambazo muathirika wa ukatili wa ngono anatakiwa kuzichuhukua ........................................ 17

**6. Sheria kuhusu Ukatili wa Kijinsia ........................................ 19**

**7. HITIMISHO ........................................ 22**

# SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa kijarida hiki hususani, Wakili Getrude Dyabene, Wakili Joanitha Mutayoba na Bi Irene Nambuo pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

# UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiaa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidiisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

# DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama wangejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengola kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi wa kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo

au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali mshirikishe na mwenzako kupata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

# UTANGULIZI

Kumekuwa na ongezeko la masuala ya ukatili hasa kwa wanawake na watoto. Taarifa nyingi za haki za binadamu zinaonesha kuwa ukatili wa kijinsia hufanyika zaidi kwa wanawake na watoto kuliko makundi mengine. Vitendo vya ukatili wa kijinsia ni makosa ya jinai yaliyoainishwa katika sheria lakini mara nyingi wahanga wa masuala ya ukatili hukosa msaada kwa kutokujua mahala salama pa kupata msaada na jinsi ya kupata haki. Upatikanaji haki katika masuala ya ukatili unakumbwa na changamoto za wanajamii kushindwa kutoa taarifa za ukatili na mara nyingine kuchelewa kufanya hivyo na kusababisha ushahidi kukosekana na hatimae haki kutokupatikana.

Pia changamoto nyingine ni watu kutokufahamu ukatili wa kijinsia ni nini, na mara nyingine makundi yanayoathiriwa zaidi hupata vitisho ili wasiweze kudai haki zao.

Kutokana na sababu mbalimbali watu wengi wamekuwa wakiathirika kutokana na vitendo ya ukatili wa kijinsia na hufika katika vyombo vya haki wakiwa wameshaathirika zaidi na wengine kushindwa hata kudai haki kwani wanakuwa wamepoteza maisha.

Ni wajibu wa kila mtu kuhakikisha anatoa taarifa kuhusu ukatili wa kijinsia katika sehemu aliyopo. Taarifa hizo zitolewe polisi katika madawati ya jinsia, kwa viongozi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na hata Kata, viongozi wa kidini au hata mashirika ya haki za binadamu.

Hutakiwi kuvumilia vitendo ya ukatili kwani vina athari kubwa zaidi, TOA TAARIFA HARAKA IWEZEKANANAVYO.

# 1. UKATILI WA KIJINSIA

## 1.1. Jinsi ni nini?

Jinsi ni hali ya kuwa na umbile la kiume au la kike.

## 1.2. Jinsia ni nini?

Jinsia hueleza tafauti za kijamii baina ya wanawake na wanaume ambazo zinaonekana kupitia mgawanyo wa kazi, upatikanaji na udhibiti wa rasilimali, mitazamo, tabia, maadili na uwezo au muundo wa kaya.

## 1.3. Maana ya Ukatili

Ni kitendo anachofanyiwa mtu yoyote chenye lengo la kumsababishia madhara au maumivu.

## 1.4. Ukatili wa Kijinsia

Kitendo chochote cha ukatili anachofanyiwa mtu kwa lengo la kumdhuru au kumuumiza kisaikolojia, kimwili, kiafya, kingono au kiuchumi kwa sababu ya jinsia yake.

Umoja wa Mataifa (UN) umetafsiri ukatili wa kijinsia kama kitendo anachofanyiwa mtu yeyote awe mwanamke, mwanaume au mtoto ambacho kimelenga kumuumiza kimwili au kiutu.

# 2. AINA ZA UKATILI WA KIJINSIA

Kuna aina tofauti za ukatili wa kijinsia;

## 2.1. Ukatili wa Kimwili

Ni kitendo anachofanyiwa mtu awe mwanaume au mwanamke kilicho na lengo la kumsababishia madhara ya kimwili kama kupigwa, kusukumwa, kuchapwa, kuchomwa moto kuporwa au kukeketwa.

## 2.2. Ukatili wa Kisaikolojia

Ni kitendo anachofanyiwa mtu (mwanamke/ mwanaume) kwa lengo la kumsababishia madhara kimawazo, kiakili au kuharibu hisia za mtu. Vitendo hivi ni kama kutukanwa, kufokewa, kudhalilishwa kwa maneno, vitendo vya ishara, kusingiziwa na kunyanyapaliwa.

## 2.3. Ukatili wa Kiuchumi

Ni kitendo anachofanyiwa mtu (mwanamke/ mwanaume) kwa lengo la kumfanya ashindwe kupata haki zake za kiuchumi au mapato.

Mfano wa ukatili wa kiuchumi ni kutomiliki mali inayokuhusu, kutokuwa na sauti katika mali inayokuhusu na kufanyishwa kazi bila malipo au kwa malipo kidogo.

### 2.4. Ukatili wa Kiafya

Ni kitendo anachofanyiwa mtu kwa lengo la kumdhuru kiafya. Mfano wa ukatili wa kiafya ni pamoja na kukosa haki ya uzazi ya kujifungulia hospitalini, maambukizi ya magonjwa kwa makusudi na kukataliwa kupata huduma za Afya.

### 2.5. Ukatili wa Kingono

Ni kitendo anachofanyiwa mtu kwa lengo la kumdhalilisha utu wake na kumletea madhara ya kimwili, kiafya na kisaikolojia. Mifano ya ukatili wa aina hii ni pamoja na kubakwa, kushikwa sehemu za mwili bila ridhaa, kulawitiwa.

# 3. SABABU (CHANZO) ZINAZOCHANGIA UKATILI WA KIJINSIA

- Mila na desturi (potofu)
- Mfumo dume
- Uelewa mdogo kuhusu sheria na haki za binadamu
- Kutokuwajibika kwa viongozi
- Imani potofu
- Elimu duni
- Ushirikina
- Umaskini
- Sera na sheria kandamizi

# 4. ATHARI ZA UKATILI WA KIJINSIA

**Kimwili**

- Ulemavu
- Madhara kimwili
- Maumivu
- Vifo
- Maambukizi ya magonjwa ya zinaa ikiwemo

UKIMWI hasa kwenye ukatili wa kingono.

- Kutetereka kwa afya
- Mimba zisizotarajiwa

**Kisaikolojia**

- Woga
- Upweke
- Kutokuamini watu wengine
- Msongo wa mawazo
- Kutokujiamini
- Kujitenga na jamii
- Magonjwa ya akili

**Kiuchumi na Kijamii**

- Kutengwa na kubaguliwa na jamii
- Kunyanyapaliwa
- Kupoteza nguvu kazi kwa jamii na nchi kiujumla.
- Kupunguza uwezo wa ushiriki katika shughuli za kijamii na kiuchumi
- Kutojiamini kwa wanawake kuwa katika sehemu za wazi kitu kinachoathiri elimu zao na hata sehemu za kazi
- Kutokuwa na uhuru

- Talaka au kuvunjika kwa familia
- Kupata watoto wasio na afya bora kutokana na ukatili aliofanyiwa mama.
- Malezi ya watoto kushuka na kuathiri watoto zaidi.
- Madhara kwa watoto wanaoshuhudia ukatili

# 5. MWONGOZO WA UTOAJI HUDUMA KWA WAATHIRIKA WA UKATILI WA KIJINSIA

- Hakikisha usalama wa muathirika na jaribu kumtuliza
- Usisogelee au kuingilia eneo la tukio ili kukwepa kuharibu ushahidi
- Mfariji muathirika kwa kumsikiliza, kumtuliza, kumpoza moyo na kumpa ushirikiano
- Kama mwathirika wa ukatili wa kijinsia ni mwathirika wa ubakaji mshauri asioge na kama inabidi kubadilisha nguo basi ahifadhi nguo hizo kwenye mfuko wa karatasi na sio kwenye mfuko wa plastiki
- Msindikize muathirika kwenye kituo cha Polisi na kituo cha afya
- Kama una taaluma ya unasihi toa nasihi ya

kupambana na kiwewe kwa muathirika na kwa familia yake

- Hakikisha shauri linafunguliwa Mahakamani ili haki ipatikane
- Upatanishi ni vyema vikafanyika Mahakamani
- Kumsaidia mhalifu wa kitendo cha ukatili wa kijinsia ni kosa la jinai na ni kuzuia upatikanaji wa haki
- Toa haraka taarifa ya kosa la ukatili wa kijinsia plae pale ambapo muathirika hawezi kufanya hivyo
- Ni vema kutoa taarifa mapema baada ya kuona, kugundua au kushuhudia ukatili wa kijinsia.

## 5.1. Hatua ambazo muathirika wa ukatili wa ngono anatakiwa kuzichuhukua

- Kukimbilia sehemu salama
- Kutafuta msaada haraka katika zahanati au kituo cha afya.
- Kuhakikisha unapewa dawa za kulinda afya na zile za kuzuia maambukizi ya zinaa (STI) na Ukimwi (PEP)
- Kutoa taarifa polisi na kuulizia dawati la jinsia
- Kuhakikisha umepewa fomu ya polisi

namba.3 (hii hutolewa bure)

- Kabla ya kutia sahihi maelezo uliyotoa polisi hakikisha umeyasoma upya na kuridhika nayo
- Kuwakabidhi polisi nguo na vitu vyovyote vilivyohusika katika tukio ili waweze kuvitumia kama ushahidi
- Kuepuka vikao ya suluhu au kutafuta mapatano nje ya Mahakama

ANGALIZO:

- Usimseme vibaya muathirika wa ukatili wa kijinsia
- Usimnyanyapae au kumbagua
- Usijadili matukio au kosa kwenye hadhara
- Usimwaibishe na kutumia maneno makali
- Usishirikiane na mtuhumiwa ili kupotosha haki kwa kuharibu ushahidi

# 6. SHERIA KUHUSU UKATILI WA KIJINSIA

i. Lugha ya matusi, mzozo na vitisho – kifungu cha 89 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kinakataza mtu yeyote kutumia lugha chafu au kutukana mtu yeyote kwa lengo la kuvunja amani. Kitendo hiki ni kosa la jinai na atakayekutwa na kosa hili atahukumiwa kifungo cha miezi sita.

ii. Unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya watoto – Kifungu cha 138B ya cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kimeainisha mazingira ambayo unyonyaji kama kosa la ukatili wa kijinsia dhidi ya mtoto linaweza kutendeka kwa mfano kumchukua au kumruhusu mtoto yeyote kukaa katika maeneo yake kwa lengo la mtoto huyo kutumiwa vibaya kwa matendo ya kujamiiana, kufanya maonyesho kinyume cha maadili, atakuwa ametenda kosa la unyonyaji unyanyasaji dhidi ya watoto

iii. Bughudha/shambulio la kijinsia – Kifungo cha 135 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 kinaeleza bayana kwamba mtu yeyote ambaye kwa dhamira akamshambulia, au akatumia nguvu kinyume cha sheria kumbughudhi mtu mwingine

kijinsia au kwa kutumia maneno au vitendo na kusababisha maudhi za ya kijinsia kwa mtu mwingine, basi mtu huyo atakuwa ametenda kosa la bughudha za kijinsia.

iv. Shambulio la aibu kwa wanawake – mtu yeyote kwa kudhamiria akasababisha maudhi ya kijinsia kwa mwanamke ama kumtamkia maneno au kutoa sauti, ishara au kuonyesha maneno au kitu chochote kwa nia kwamba maneno hayo au sauti hiyo iweze kusikika au ishara au kitu hicho kiweze kuonekana na mlengwa, basi mtu huyo atakayefanya moja kati ya maudhi hayo atakuwa ametenda kosa la shambulio la kijinsia na shambulio la aibu kwa wanawake.

v. Makosa ya maharimu kwa wanaume – mwanaume yeyote ambaye atakuwa na mahusiano ya kujamiiana na mwanamke huku akifahamu kuwa ni ndugu yake wa karibu kama vile mjukuu wake, binti yake, dada au mama yake basi kisheria atakuwa ametenda kosa la maharimu kwa wanaume.

vi. Makosa ya maharimu kwa wanawake – mwanamke yeyote mwenye umri wa miaka 18 au zaidi ambaye

kwa ridhaa yake atamruhusu babu yake, baba yake, kaka au mtoto wake wa kiume kujamiiana naye, basi kisheria atakuwa ametenda kosa la maharimu kwa wanawake

vii. Kosa la kutena na kukeketa - kifungu cha 169A cha sheria ya Kanuni ya za Adhabu, sura ya 16 kinatoa kosa kwa mtu yeyote ambaye ana dhamana ya kumtunza au mwangalizi wa mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18, kumtesa, kutelekeza au kumkeketa ama kupelekea mtu huyo kuteseka, kuteswa au kutelekezwa kwa lengo la kudhuru afya yake..

ANGALIZO

Vitendo vingi vinavyotambulika kama ukatili wa kijinsia ni makosa ya jinai au husababisha makosa ya jinai ambapo mengi huadhibiwa kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 ya sheria za Tanzania. Lakini pia kuna makosa mengine ambayo ni kosa la daawa (madai) na mengine yanadondokea kuwa kama makosa ya jinai na daawa kama kitendo cha

kumdhihaki mwanamke ambalo ni kosa la jinai pia ni daawa.

ANGALIZO

Sheria za Tanzania ingawa hazijataja kosa la ukatili wa kijinsia kama kosa la jinai, makosa mengi ya ukatili wa kijinsia huangukia katika makosa ya jinai. Kwa mujibu wa sheria katika makosa ya jinai kutokujua sheria sio utetezi hivyo basi hata kama mtu akafanya ukatili wa kijinsia bila kujua kwamba ni kosa bado atakamatwa na kupelekwa mbele ya Mahakama

## 7. HITIMISHO

Msomaji wetu, ni matumaini yetu kwamba mpaka sasa unajua maana ya Ukatili wa Kijinsia na wapi pa kutoa taarifa pale unapofanyiwa ukatili au pale unapoona mwenzako anafanyiwa ukatili. Ni muhimu kuhakikisha kuwa vitendo vya ukatili vinatolewa taarifa kituo cha polisi na sio kusuluhisha majumbani kwani vitendo hivi ni vitendo vya jinai na suluhu yake hupatikana Mahakamani.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**DODOMA OFFICE**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Barabara ya Olerian, Olosiva Kitalu Na. 116/5,
Sakina kwa Idd, Arumeru
S. L. P. 15243, Arusha - Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*